Ebola

Ebola ni nini?

Ebola ni ugonjwa wa kweli ambao umeua maelfu ya watu Afriica ya mngaribi, ya Mashariki na Africa ya kati kwa miaka yakupita. Kwa wakati huu, Ebola imejitokeza kwa kishindo kikubwa kwa Africa ya Mangaribi na imetapakaa kwa nchi nne. Imewaua maelfu ya watu. Kwa wakati huu, kumeonekana Ebola katika jamhuri ya kidemocracia ya D R Congo, ugonjwa wa ebola usiofanana nahuo wa Africa ya mangaribi umejitokeza. Tukijua uhusu ugonjwa huu na namna ya kujikinga, ni jambo la muhimu kuwatayarisha kujikinga na kuwaweka shwari, ninyi mulio wapendwa wetu.Kwa sababu ya hiyoo soma yafuatayo na uelezee watu wengine mujini mwenu. Hata kama ugonjwa huu haujajitokeza kwa maeneo yenu, ni jambo la maana kwako ao kwenu kujua mambo haya ili ugonjwa upya usijitokeze kwa maeneo yenu. Fuata muongozo wa serekali, wa wafanyakazi wa afya ao shirika yoyote inayo saidia kutayua ugonjwa huu usisambazwe kwa watu wengine ao maeneo mengine.

Ebola haitokane na pepo wabaya ao ulozi lakini kwa kirusi kidogo sana. Kirusi hicho cha Ebola ni kiini kidogo sana kwa kuona na macho ndani ya mwili, damu ao maji mengine mwilini mwa mtu. Mtu anaweza kuambukizwa kutoka wagonjwa wengine, vyombo wagonjwa wengine waligusa, ao kutoka kugusa ao kukula wanyama. Huo ugonjwa unaua zaidi ya nusu ya wanao ambukizwa virusi. Hakuna tiba kwa ugonjwa lakini watu wamoja wanaishi kwa musaada wa Mungu kupitia matunzo ya dawa. Shirika nyingi za dawa ziko zinatumika kwa kupata tiba lakini inachukua mda. Tunaweza kujikinga kwa kutokupata na kutawanya virusi, lakini sharti tufuate maongozi na maonyo ya wataalamu wafanya kazi wa afya mtu anpoambukizwa Ebola.

Dalili zinazo onyesha mtu ana virusi vya Ebola ni gani?

Mtu baada ya kuwa na mgonjwa ya ebola hupata ao huambukizwa baada siku 2 ao 21.

Dalili za mwanzo ni pamoja na**:** maumivu gafla ya homa na mishipa ao misuli, homa ya gafla(38.6°C), maumivu ya hicha, maunganio na misuli, vidonda kati ya koo/shingo, na uzaifu ya kupindukia.

Dalili za ufuata(avanc) ni pamoja na**:** kuhara na ao kytapika(inakuwa nyeusi ao na tone za damu,) kujikuna, maumivu ya figo na maini,nna estomac.

Wagonjwa wamoja wanaweza kuwa na**:** mecho mekudu, sekuseku, kuchubuka mwili ao ngozi, kwa urahisi na kutoka damu.

Watu wanapata ugonjwa wa Ebola namna gani?

***Kutoka wanyama kwa watu*:** njia ya kwanza watu wanapatawa na Ebola ni kwa kushika, kuchinja, ao kupika nyama mbichi ya porini inayokuwa na virusi ya Ebola.

- Unaweza kupata virusi kupitia kidonda ao kuumizwa juu ya ngozi yako inayo gusa mnyama.
- Ukigusa mnyama anayeambukizwa kisha uguse kinywa chako, pua ao macho; virusi vinaweza kupita kutoka mnyama kupitia vidole yako kisha kwa mwili wako

- Ukila nyama mbichi ao ya kukauka ao damu ya mnyama aliye na virusi kuingia kwa mwili wako.
- Usiguse ao kukula nyama ya mnyama anayekuwa mgonjwa wa Ebola ao mnyama aliyekutwa amekufa.
- Ukigusa ao kula tunda ambalo limekuliwa nusu na mnyama aliyambukizwa sawa popo unaweza kuambukizwa vile na virusi.

- Wanyama wanaochukua virusi vya Ebola ni kama sokomtu, kima,panya, swala,, uambwa, nguruwa,popo, nungu (porc-epic) dudu (kulungu ao ayala).
- Haiwezekani kuambukizwa kutokana na nyama iliyopikwa vizuri.

Ku*toka mtu mmoja kwa mtu mwengine*: Kuambukizwa kunaanza wakati mtu mmoja anapopatwa na Ebola kutoka mnyama na kupitishia virusi kwa watu wa jamaa yake, marafiki na watu wengine wanaokuwa karibu naye akiwagusa wanapokuwa wagonjwa ao baade ya kufa kwao.

- Ukigusa mtu anayekuwa na Ebola unaweza kuambukizwa.
- Ukigusa maji yanayotoka mwilini mwa mtu anayeambukizwa na virusi vya Ebola unaweza kupata Ebola
- Maji yote yanayotoka mwilini mwa mgonjwa wa Ebola yanabeba virusi. Ni kama damu, jasho, machozi, na mate, mbegu za uzazi kutoka viungo vya uzazi, mkojo, mavi, ao matapishi/matapiko.



- Virusi vya Ebola vinaweza kuendelea kuwa katika mbegu za uzazi ao kutoka katika viungo vya uzazi vya mwanamuke na mwanaume, na katika makojoo kwa muda wa siku tatu baada ya uponyaji.
- Unaweza kuambukizwa ugonjwa wa Ebola ukigusa nguo zilizochafuliwa na mgonjwa wa Ebola, kutoka kitanda chake, matandiko ya kitanda ao malalo (mkeka, godoro, nguo, majani…) vile kugusa shindano ao wembe ya mtu aliyeambukizwa.
- Unaweza kuambukizwa Ebola kwa kugusa mwili wa mtu aliyeambukizwa na ugonjwa wa Ebola.
- Desturi za kuosha mwili wa mtu aliyekufa na ugonjwa wa Ebola ni njia ya kwanza watu wengine wanaambukizwa ugonjwa wa Ebola.

Namna gani kujikinga na ugonjwa wa Ebola?

- Kujiadibisha na kuadibisha wengine kuusu ugonjwa wa Ebola ni kwa mhimu sana kujikinga ao kwa kinga.
- Serekali ya D.R Congo imetoa Sheria wa kutokusalimiana kwa mikono kwa mikono kwa wakati Ebola inavuma, kwa sababu ya kujitokeza kwa sasa mkasa wa Ebola katika Africa ya mangaribi na katika Kaskazini mangaribi mwa Congo.

- Serkali ya Congo imetoa vilevile sharia ya kuosha kila mara mikono na sabuni na maji safi na kuchunga binafsi usafi na afya.
- Kuepuka kutembelea mahali ugonjwa wa Ebola unaonekana kwa wakati huu.
- Kuepuka mikutano mikubwamikubwa za watu kunapo kuwa uweekano wa kuambukizwa ugonjwa wa Ebola.
- Kupika nyama vizuri wakati wowote, hata wakati Ebola haijaonekana katikati yenu wala kwa maeneo munamokaa.
- Tumia vyombo sawa mifuko ya mikono (gants) kwa kukinga mikono yako unapotaka kugusa mtu anayezaniwa, (kushukiwa) kuwa na ugonjwa wa Ebola.
- Vaa nguo zingine baada ya kugusa nyama ya porini.
- Usiguse wala kuosha watu waliofariki kutokana na ugonjwa wa Ebola.

- Ruhusu wafanyakazi wa huduma ya afya kusafisha maambukizi ao kuzika mwili wowote unaoshukiwa kufa kwa ugonjwa wa Ebola. Mwili huu uzikwe haraka bila kukawia na wataalamu kuhusu ugonjwa wa Ebola.
- Shirikiana na kikundi chochote cha serkali cha afya ao cha police kuzuia usambazaji ao kuambukizwa kwa ugonjwa.Kikundi hicho kinahakikisha kinasimamisha kwa mda kuhamahama kwa watu (ao kwa wanyama) wanaokuwa na virusi ao wanaoweza kuwa wameambukizwa kwa lengo la kukinga kusambazwakwa ugonjwa.

Nini ifanyike ikiwa Ebola imeshukiwa(kuzaniwa) kuwa eneo

- Omba Mungu na kumuuliza alete uponyaji na ulinzi kwa wewe na wapendwa wako.
- Ujiepushe kushirikkiana na wengine. Tafuta usaidizi na muongozo kutoka viongozi (si kwa kila mtu)
- Nenda kwa kituo cha afya kilicho karibu nawe. Uwaonye mara moja ya kwamba inaweza kuwa Ebola na ya kwamba unahitaji kuangaliwa (kuchunguzwa, ao kuhakikisha).
- Usiende kwa waganga wa kyenyezi ao wa dawa ya miti shamba.—hawawezi kukusaidia.
- Usijaribu kuwachunga watu wanaokuwa na dalili ya Ebola katika nyumba yako ao katika eneo lako ila tu ikiwa umepata kwanzaagizo kutoka wafanya kazi wa idara ya afya.
- Usichunge ugonjwa wa Ebola kwa siri kwa viongozi. Kuchunga siri hakutasaidia mtu kupona lakini itahatarisha jamaa lako na watu wengine.
- Saidia viongozi kuzibitisha/kugundua mtu yeyote anayeweza kuwa na virusi ao ambaye alikuwa katika maeneo yanayokuwa na virusi.
- Magonjwa yanayoletwa na virusi vya Ebola yanaweza kuzibitishwa tu katika nyumba ya kufanyiwa uvumbuzi wa dawa na machine (laboratoire).
- Kutengwa kwa mgonjwa na matunzo/matibabu ya wataalamu tu inaongeza uwezekano ao bahiti ya kuishi tena.

Tumaini kwa wale wanaoteseka na ugonjwa wa Ebola

Mungu anapenda kila mmja wetu kwa kimwili na kiroho. Mungu angali anaendelea kufanya kazi katika maisha yetu hata wakati mtu anashikwa na ugonjwa wa Ebola. Mungu anaweza kutumika kupitia magonjwa kufungua macho yetu kwa haja yetu ya

kiroho. Na jinsi Ebola inaweza kuleta kifo , zambi zetu zinaleta vile kifo cha kiroho na kutututenga na Mungu muumba wetu.watu wanaweza kupona kutoka Ebola kkupitia matunzo ya kiafya (dawa) na kupitia msaada wa Mungu. Lakini njia moja kupona kifo ya kiroho ni kupitia uhusiano na Kristo. Biblia inasema ya kwamba zambi inatutenga na Mungu (Rom 3.23).lakini Mungu alionyesha upendo wake mkubwa kwetu tangu wakati Yesu alipokufa kwa ajili ya zambi zetu wakati tulipokuwa wenye zambi (Rom 5.8). kutoka Biblia tunasoma kwamba tukitubu kwa vinywa vyetu ya kwamba Yesu ni bwana wa uzima wetu na kuamini katika roho ya kwamba Mungu alimfufua toka wafu, tutaokolewa (Rom 10.9-10). Tukiishi ao tukikufa kwa wakati huu yajulikana na Mungu tu. Lakini tunaweza kufarijuwa tukijua ya kwamba wale wanaokufa wakijua Yesu Kristo wataenda pamoja naye mbinguni wakifa. Tunaomba utapata salama na tumaini kumjua Yesu kama Bwana na Mwokozi wako binafsi. Maombi yetu ni kwamba tukitawanya habari kuhusu Ebola watu wengi watapata msaada wa kiafya (medica) Ebola na amekombolewa toka kituo cha afya anapashwa kukaribishwa vizuri katika jamii kwa sababu hawezi tena kuambukiza magonjwa ya Ebola, kwa neema ya Mungu wanaishi tena.

Chanjo ya Ebola kwa sasa

***DR Congo*:** mama mujamuzito kutoka muji wa kanamongo, District ya Boende Province ya Equateur, alipata ugonjwa wakati alipochinja nyama ya porini ambayo mme wake alimletea. Alipoenda kwa kituo cha afya akawaambukiza dactari na wauguzi (infirmiers) kwa sababu hawakujua ni Ebola huyo mama alifariki tarehe 11/ 09/ 2014 mpaka pale watu 62 wameambukizwa ugonjwa wa Ebola, katika miji mine na watu 35 wamefariki miongoni mwao. Watu wapatao 386 wanashukiwa kuwa walihusika kwa njia moja ao ingine na ugonjwa wa Ebola. Hiyo ni tukio la saba tangu ilipoonekana Congo mara ya kwanza kwa mwaka 1976. Aina hii ya Ebola si hiyo inayoonekana kwa Africa ya Mangaribi.

***Guinea, Africa ya Mangaribi*:** Tukio hili katika Afria Mangaribi ilianza na motto wa miaka miwili aliyefariki tarehe 6/12/2013. Baadaye mamaye, tate wake wa kike, na dada yake wakafa na ugonjwa pia. Tangu tarehe 7/09/2014 ugonjwa umeua watu 557 katika Guinea. Na imesambazwa katika miji yenye watu wengi sana katika inchi ine: Liberia (vifo 1137), Sierra Leone (vifo 524), Nigeria (vifo 8), and Senegal (kifo 1 hadi sasa).

***Sierra Leone, Africa Mangaribi*:** ugonjwa umetapakaa inchini Sierra Leone kwa sababu mganga wa kienyeji (devin) alijidai kuwa na uwezo wa kipekee wa kutibu na kuponyesha ugonjwa. Watu wenye ugonjwa wa Ebola wakasafiri kutoka Guinea mpaka Siera Leone kuona huyo mwanamke muuguzi mwenye uwezo. Naye akapatwa na ugonjwa na akafariki tarehe 26/05/2014. Kwa mazishi yake wanawake wakagusa mwili wake na baadaye wakafariki pia kwa Ebola. Baada ya hiyo ugonjwa ukazidi na kutawanyika. Hii inaonyesha gisishetani anaweza kutumia pepo mbaya, ulozi na uchawi kuleta mateso mengi na vifo kupitia mafundisho ya uongo ya kidini.

***Nigeria*:** kijana kutoka Nigeria akafariki na Ebola alipotembelea Liberia. Baba yake akapatwa na ugonjwa pia na akarudi Nigeria tarehe 20/07/2014. Mtembeza gari aliyemchukua kutoka uwanja wa ndege akafa naye pia vile madactari na wauguzi waliomutibu.

Copyright © September 2014 Equip Disciples